# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# KITINI CHA MAFUNZO YA UANDAAJI WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA (GENDER RESPONSIVE BUDGETING)

**2026**

Wizara ya Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
Mtaa wa Afya, Mji wa Serikali, Mtumba.
P.O. Box 573, 40478 Dodoma, Tanzania.

Huduma kwa Wateja:
0734 986 503 / 0262 160 250
0766 400 168 / 0769 608 130

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **VIFUPISHO VYA MANENO** | **3** |
| **DIBAJI** | **4** |
| **MUHTASARI** | **6** |
| **SHUKRANI** | **7** |
| **SURA YA KWANZA – MWONGOZO WA JUMLA KWA MWEZESHAJI** | **8** |
| Lengo mahsusi la kitini | 8 |
| Matokeo Yanayotarajiwa baada ya mafunzo | 8 |
| Sifa za mwezeshaji | 9 |
| Nyenzo za kufundishia | 9 |
| Ufunguzi wa Mafunzo | 9 |
| Mbinu za ufundishaji | 10 |
| Vidokezo/dondoo za jumla kwa mwezeshaji | 10 |
| Mwisho wa Mafunzo | 11 |
| Muda wa mafunzo | 11 |
| **SURA YA PILI - MUKTADHA WA SERA NA DHANA ZA JINSIA** | **12** |
| Muktadha wa sera | 12 |
| Ufafanuzi wa dhana za kijinsia na mahusiano yake katika bajeti | 12 |
| **SURA YA TATU - UKONDOISHAJI WA MASUALA YA KIJINSIA KATIKA MIPANGO NA BAJETI** | **20** |
| MAANA YA NENO BAJETI NA DHANA MBALIMBALI ZA BAJETI | 20 |
| UMUHIMU WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA | 21 |
| KANUNI ZA UPANGAJI WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA | 22 |
| HATUA KWA HATUA KATIKA UANDAAJI WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA | 23 |
| **SURA YA NNE – MPANGO KAZI** | **35** |
| Mpango kazi | 35 |
| Hitimisho | 35 |

# VIFUPISHO VYA MANENO

AZAKI ...................Asasi za Kiraia

CMT .....................Council Management Team

DCC .....................District Consultative Committee

DPP .....................Director of Policy and Planning

GBV .....................Gender Based Violence (Ukatili wa Kijinsia)

GEWE ..................Gender Equality and Women Empowerment
(Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake)

GRB .....................Gender Responsive Budgeting (Bajeti yenye Mrengo wa Kijinsia)

FYDPs ..................Five Years Development Plan

KAGIS ...................Keeping Adolescent Girls in School

M&E ..................... Monitoring and Evaluation

MTAKUWWA ........Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto

NACTVET .............National Council for Technical and Vocational Education Training

NBS ......................National Bureau of Statistics (Ofisi ya Taifa ya Takwimu)

NGOs ................... Non Governmental Organisations (Asasi zisizokuwa za Kiserikali)

RCC .....................Regional Consultative Committee

SIGI ......................Social Institutions and Gender Index

TAMISEMI ............Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

TCU ......................Tanzania Commission for Universities

TDHS ....................Tanzania Demographic and Health Survey

TGNP ....................Tanzania Gender Networking Programme

TEHAMA ...............Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

UN Women ........... United Nations for Women

VEOs .....................Village Executive Officers (Watendaji wa Vijiji)

WEOs ....................Ward Executive Officers (Watendaji wa Kata)

# DIBAJI

Juhudi za kuzingatia mitazamo ya kijinsia katika bajeti za kitaifa nchini Tanzania, zilianza tangu miaka ya 1980. Mwanzoni jitihada hizo ziliitwa "bajeti ya wanawake"; Baadaye ziliitwa "bajeti za kijinsia" ili kuendana na mabadiliko yanayoendelea kutoka mtazamo wa wanawake hadi kuzingatia jinsia na uhusiano kati ya wanawake na wanaume. Neno lingine linalotumiwa kwa kawaida ni "bajeti nyeti za kijinsia". Hivi karibuni kuna matumizi mapana ya neno "kuingiza na kuzingatia masuala ya kijinsia katika bajeti za kitaifa", ambayo ni neno sahihi zaidi kwani lengo sio kutengeneza bajeti tofauti ya kijinsia lakini kuingiza masuala ya kijinsia katika michakato ya bajeti za kitaifa. Hiyo inaakisi masuala ya kijinsia kuanzia kwenye muundo, upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini kwenye taasisi.

Nchini Tanzania, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa), hasa ibara ya 12, inaweka msingi wa kisheria wa usawa kati ya wanaume na wanawake *"kwamba Serikali na taasisi/mashirika yake yote yanatoa fursa sawa kwa wananchi wote, wanaume na wanawake bila kujali rangi zao, kabila, dini, au maeneo ya makazi"*. Aidha, bajeti inayozingatia usawa wa kijinsia ni tamko la sera kuhusu usawa wa kijinsia, Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2050 , Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia 2021/22-2025/26 na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake 2023, Mikakati na mipango ya utekelezaji wake, imebainisha mapungufu katika ugawaji wa rasilimali ili kufikia malengo ya sera. Kwa kutambua suala hili kumeisaidia Serikali kuandaa mifumo ya kisheria na sera pamoja na mikakati inayosaidia ujumuishaji wa jinsia katika michakato yote ya maendeleo. Tanzania imeridhia mikataba na matamko mbalimbali ya kimataifa na kikanda ya kuleta usawa kwa wanawake na wanaume.

Aidha, Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa maelekezo ya kuzingatia wakati wa maandalizi ya mipango na bajeti kupitia Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kila mwaka. Mwongozo huo unabainisha masuala ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Ofisi za wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za mipango na bajeti. Miongoni mwa masuala ya kuzingatiwa ni ushirikiano wa kikanda na kimataifa; Masuala ya watu wenye ulemavu; masuala ya kijinsia na masuala mtambuka.

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023) imeainisha maeneo makuu matatu ya kuzingatia katika kuleta usawa wa kijinsia ambayo ni; (i) Uwezeshaji wanawake kiuchumi, (ii) Kutokomeza ukatili wa kijinsia, (iii) Ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na nafasi za maamuzi.

Kadhalika, katika uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia (Gender Responsive Budgeting), Maafisa Masuuli wanaelekezwa: K utambua m asuala y a k ijinsia k atika m aeneo y ao kwa kufanya uchambuzi wa takwimu ili kutekeleza hatua za kukabiliana na upungufu uliobainika katika taasisi husika; Kutekeleza Mpangokazi wa Pili wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II 2024/25 – 2028/29); Kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu inayozingatia jinsia; na Kutenga bajeti kwa ajili ya mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Kitini hiki cha mafunzo ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia ni nyenzo ya kumuongoza mwezeshaji kujua makusudio ya mafunzo na kutoa mafunzo yanayokusudiwa katika viwango stahiki. Kitini pia kinaweza kutumika kama nyezo rejea kwa watu wote ambao wanahusika katika mchakato wa bajeti ili kujikumbusha mambo muhimu ya kuzingatia katika uandaaji wa

bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Kitini kina sehemu kuu nne, ambapo sehemu ya kwanza imebeba maelekezo ya jumla kwa mwezeshaji/mkufunzi, sehemu ya pili imebeba elimu ya masuala ya jinsia kwa kina, sehemu ya tatu inaelezea masuala ya kijinsia yanavyotakiwa kuzingatiwa katika uandaaji wa bajeti na sehemu ya nne inabeba dhana ya wafundishwaji kujaribu kuyaweka mafunzo kwa vitendo kwa kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia na kuweza kuipima kwa kuona mambo ya msingi ya kijinsia yakiwa yamezingatiwa.



# MUHTASARI

Kuhusisha masuala ya kijinsia katika bajeti za kitaifa umekuwa mjadala mkubwa katika taasisi mbalimbali duniani kote. Tanzania inatambua jinsia kama suala la kimaendeleo na kwamba ukosefu wa usawa wa kijinsia katika jamii unazuia makundi mbalimbali kutambua fursa zilizopo katika shughuhuli za kimaendeleo hususani katika nyanja ya uchumi, siasa, na huduma za kijamii kama vile afya, elimu, miundombinu, biashara na maji.

Kuonyesha dhamira ya dhati katika kuwa na bajeti yenye mrengo wa kijinsia, Wizara ya Fedha kwa miaka kadhaa sasa imekuwa ikitoa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kila mwaka, ikisistiza bajeti zote zinazoandaliwa na mafungu ziwe zenye mrengo wa kijinsia. Mfano mzuri ni Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 katika ukurasa wa 36 ambapo Serikali imesisitiza kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia na kutenga bajeti ya mafunzo ya uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Katika kuendeleza dhamira hiyo Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali imeandaa kitini cha mafunzo ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia. Kitini hiki kinaeleza mbinu na mikakati ya kina ya kuwezesha mafunzo kwa wadau wote wanaohusika katika mchakato wa uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia, kinaonyesha umuhimu wa kutumia mbinu mbalimbali za mafunzo kama vile mazoezi ya vitendo, tathmini za awali na tathmini baada ya mafunzo na mbinu shirikishi ili kuboresha uzoefu wa kujifunza kwa washiriki na kutoa ufafanuzi kuhusu dhana, kanuni na bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Lengo la Kitini hiki cha mafunzo ni kuwajengea uwezo Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Ofisi za wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na mashirika ya Umma, na watu wote wanaohusika katika maandalizi, utekelezaji ufuatiliaji na tathmini na utoaji wa taarifa za mipango na bajeti.

Ni matumaini ya Serikali kuwa, kupitia mafunzo yatakayokuwa yanatolewa kupitia kitini hiki, tutapata matokeo chanya katika hatua ya maandalizi, upangaji na utekelezaji wa bajeti zenye mrengo wa kijinsia na hivyo kufikia adhima ya kuhahakikisha kila mtanzania anapata haki yake pasipo kujali jinsia yake.




**Dkt. Natu El-maamry Mwamba**
Katibu Mkuu,
Wizara ya Fedha.



# SHUKRANI

Maandalizi ya kitini cha Mafunzo ya Uandaaji wa Bajeti yenye mrengo wa kijinsia kwa Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Ofisi za wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma yamefanyika kwa ushirikiano kati ya Wizara za Kisekta na wadau wa masuala ya Usawa wa Kijinsia kutoka maeneo mbalimbali nchini Tanzania. Hatua za maandalizi ya kitini hiki zinajumuisha tathmini ya Mipango na Bajeti kwenye Halmashauri zilizofikiwa, kupitia nyaraka na miongozo mbalimbali, maoni na mapendekezo ya wadau, pamoja na kuandika kitini chenyewe. Hivyo, Wizara inatoa shukrani za dhati kwa watu, wadau, Taasisi, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Wizara zote zilizoshiriki kwa namna moja au nyingine kutumia muda, ujuzi na fedha kufanikisha uandaaji wa kitini hiki.

Aidha, Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Shirika la Plan International kupitia ufadhili wa Serikali ya Watu wa Canada kwa kushirikiana na Wizara za kisekta kuandaa kitini hiki cha mafunzo ya uandaaji wa mipango na bajeti yenye mrengo wa kijinsia ili kitumike kuwajengea uwezo maafisa na watendaji wote wakati wa maandalizi, upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za mipango na bajeti yenye mrengo wa kijinsia. Aidha, Serikali inayashukuru Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Tanzania Gender Networking Programme (TGNP), Policy Forum, UN-Women Tanzania, European Union (EU) kwa ushiriki wao katika kuandaa Kitini hiki. Pia Serikali inawashukuru maafisa na wadau wote walioshiriki katika tathmini ya mipango na bajeti katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, watu na wadau wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha maandalizi ya kitini hiki. Aidha, Serikali inawapongeza na kuwashukuru wataalam wote kutoka Wizara za Kisekta kwa utayari wao na kutoa utaalam wao uliowezesha kukamilika kwa kitini hiki.

Mwisho, Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Wizara zote za kisekta kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Wizara katika kufanikisha uandaaji na utekelezaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Asante Sana.

**Dkt. John A . K Jingu**
Katibu Mkuu,
Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

# 1. SURA YA KWANZA – MWONGOZO WA JUMLA KWA MWEZESHAJI

Katika sehemu hii, mwongozo wa jumla unatolewa kwa mwezeshaji juu ya masuala ya kuzingatia na kuandaa katika kutoa mafunzo ya ukondoishaji wa masuala ya jinsia katika mchakato mzima wa bajeti. Vilevile malengo mahsusi ya kitini yameelezewa yakiwa na lengo la kumuongoza mwezeshaji kuelewa kile kinachokusudiwa kufikiwa ili kutotoka nje ya mada zinazohusika. Sifa za Mwezeshaji zimeelezewa kwa kina ili kuwa na mtu sahihi ambaye ana uelewa mpana katika masuala ya kijinsia, bajeti na kuweza kujibu na kutoa mwongozo kwa wafundishwaji ambao utawaongoza kuyatumia mafunzo katika mchakato mzima wa bajeti. Mwisho kabisa wa sehemu hii inasisitiza mbinu mbalimbali za mafunzo kutumika ili kuweza kuwachangamsha wafundishwaji, kuwawezesha kushirikisha uzoefu wao na kuelewa kwa haraka.

Kitini hiki ni nyenzo muhimu na kinatumiwa na watekelezaji wote katika utekelezaji wa takwa la kibajeti ambalo linahimiza bajeti zote zinazoandaliwa Tanzania Bara ziwe zimeandaliwa kwa kuzingatia mrengo wa kijinsia.

## 1.1 Lengo mahsusi la kitini

i. Kutoa mwongozo kwa mwezeshaji wakati wa utoaji wa mafunzo ya ukondoishaji na uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

ii. Kutumika kama nyenzo rejea wakati wa maandalizi ya mipango na bajeti.

## 1.2 Matokeo Yanayotarajiwa baada ya mafunzo

i. Kuwa na uelewa na mbinu za pamoja katika ukondoishaji na upangaji wa mipango na bajeti yenye mrengo wa kijinsia kwa watu wote wanaohusika moja kwa moja au kushiriki katika mchakato wa bajeti.

ii. Kuwa na uwiano wa kitaifa katika ukondoishaji na uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

iii. Kuwa na Taifa lenye usawa wa kijinsia na maendeleo jumuishi.

## 1.3 Sifa za mwezeshaji

i. Awe na uelewa mpana wa dhana za jinsia na upangaji wa bajeti unaozingatia usawa wa kijinsia.

ii. Awe na uelewa wa uchambuzi na matumizi ya takwimu zilizonyambulishwa kijinsia.

iii. Awe na uelewa wa matumizi na zana za upangaji wa bajeti unaozingatia usawa wa kijinsia.

iv. Awe na uelewa wa michakato, miundo, na wadau muhimu wakati wa uandaaji wa bajeti.

v. Awe na uelewa wa mchakato wa bajeti katika ngazi, na taasisi mbalimbali za Serikali.

vi. Awe na uelewa wa masuala ya usawa wa kijinsia katika mipango na matumizi ya fedha za umma.

vii. Awe na uwezo wa kufundisha kwa kuzingatia utofauti wa kitamaduni katika masuala ya kijinsia.

## 1.4 Nyenzo za kufundishia

Wakati wa maandalizi ya mafunzo, mwezeshaji aandae nyenzo/vifaa mbalimbali ambavyo atavitumia wakati wa mafunzo. Nyenzo hizo ni kama,

i. Michoro au picha

ii. Video fupi/kisa mafunzo

iii. Projector

iv. Karatasi za maandishi (flipcharts)

v. Kalamu za rangi (markers)

vi. Gundi ya karatasi n.k.

## 1.5 Ufunguzi wa Mafunzo

Wakati wa ufunguzi wa mafunzo, mwezeshaji aanze kwa kutoa nafasi ya yeye kujitambulisha, washiriki kujitambulisha, washiriki kueleza matarajio yao baada ya mafunzo, lengo la mafunzo, kanuni za kuongoza mafunzo, mbinu zitakazo tumika katika mafunzo na utangulizi mwingine wowote wa jumla.

## 1.6 Mbinu za ufundishaji

Katika uwasilishaji wa mada mbalimbali zinazofafanuliwa katika kitini hiki, Mwezeshaji atumie mbinu mbali mbali katika ufundishaji kulingana na aina ya washiriki alionao. Mbinu zinazoweza kutumika ni;

**Mhadhara** | **Majadiliano Ya Kikundi** | **Kisa Mafunzo** | **Kuigiza**

Ni muhimu mwezeshaji kutumia mbinu mbili mpaka tatu katika uwasilishaji wa kila mada ili kuleta ushiriki na ushirikishwaji chanya kwa wafundishwaji. Mwezeshaji ahakikishe kwamba anakuwa na mchanganyiko wa vikundi unaobadilika kila wakati ili washiriki wote wapate kushirikiana angalau mara moja wakati wa mafunzo. Mwezeshaji atatumia fomu za tathmini kabla na baada ya mafunzo ili kupima uelewa wa washiriki.

**Msisitizo**

**Wakati wote wa mafunzo, mwezeshaji ahakikishe kwamba uwasilishaji wa mada unakuwa shirikishi na unatumia kanuni za elimu ya watu wazima kama vile heshima, mifano halisi, muda nk.**

## 1.7 Vidokezo/dondoo za jumla kwa mwezeshaji.

i. Andaa wasilisho/mawasilisho kabla ya kufanya mafunzo.

ii. Andaa mazoezi na mifano ya kisa mafunzo kabla ya mafunzo.

iii. Andaa fomu za tathmini kabla ya mafunzo.

iv. Wakati wa mafunzo andaa chati ya matarajio ya washiriki na uibandike ukutani wakati wote wa kipindi kwa ajili ya marejeleo.

v. Zungumza kwa sauti wakati wote.

vi. Wachangamshe washiriki kwa mazoezi mafupi mafupi katikati ya mafunzo.

vii. Shirikisha washiriki zaidi ili kupata mifano halisi katika mazingira yao.

viii. Zingatia muda uliopangwa/mliokubaliana kwa siku, kwa zoezi fulani au kwa mada fulani.

## 1.8 Mwisho wa Mafunzo

i. Karibisha majadiliano ya wazi na toa ufafanuzi unaohitajika.

ii. Waombe washiriki kuelezea muhtasari wa mambo makubwa waliyopata kutoka kwenye mafunzo.

iii. Rejea matarajio yaliyoainishwa na washiriki wakati wa kuanza mafunzo na kuona ni kwa kiwango gani matarajio hayo yame ikiwa.

## 1.9 Muda wa mafunzo.

i. Muda unaotarajiwa si chini ya masaa sita kwa siku.

ii. Mafunzo haya yatakuwa ya siku tatu mfululizo kulingana na aina ya washiriki.

# 2. SURA YA PILI – MUKTADHA WA SERA NA DHANA ZA JINSIA

Sura hii ina sehemu kuu mbili, sehemu ya kwanza inaelezea muktadha wa sera katika ukondoishaji na uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia na sehemu ya pili inaelezea dhana muhimu za jinsia katika ukondoishaji na uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

## 2.1 Muktadha wa sera

i. Katika kuandaa mipango na bajeti maafisa/watekelezaji husika wataongozwa na sera, mipango, mikakati na viashiria vya kitaifa vya usawa wa kijinsia kama zifuatazo;

ii. Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050

iii. Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2026

iv. Sera ya Maendelo ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023)

v. Mikataba ya Kikanda na Kimataifa

vi. Sera mahsusi za kisekta

Sera, mipango na viashiria hivi vinaainisha mahitaji na vipaumbele katika kufikia malengo ya usawa wa kijinsia na maendeleo jumuishi.

## 2.2 Ufafanuzi wa dhana za kijinsia na mahusiano yake katika bajeti.

Katika sehemu hii mada ya dhana za jinsia zitajadiliwa kwa mapana yake ikiwa na lengo kuu la kumuongoza mwezeshaji kuwajengea uelewa washiriki katika dhana za jinsia na mahusiano yaliyopo katika ukondoishaji na uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

### 2.2.1 Jinsi;

Ni hali ya kimaumbile inayotofautisha mwanaume na mwanamke ambayo mtu huzaliwa nayo. Tofauti za kijinsi ni za kibaiolojia na hazibadiliki ulimwengu wote.

### 2.2.2 Jinsia;

Mgawanyo wa majukumu baina ya wanawake na wanaume katika jamii. Mgawanyo huo unatokana na mitazamo iliyojengeka ndani ya jamii husika ambapo majukumu hayo yanaweza kutofautiana kulingana na muda au baina ya jamii moja na nyingine.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** dhana hii inasaidia kubaini mapungufu ya mgawanyo wa majukumu na mahitaji kutokana na jinsi na jinsia. Dhana hizi ndio msingi wa mjadala wa mzigo wa kazi, haki na usawa katika jamii nk.

**Tofauti kati ya jinsi na jinsia**

| Jinsi | Jinsia |
|---|---|
| Kibaiolojia | Imeundwa kijamii |
| Ulimwengu wote | Tofauti kwa kila utamaduni |
| Ya kuzaliwa nayo | Inafunzwa |
| Haiwezi kubadilika | Inabadilika kutokana na muda |
| Miili tofauti | Thamani isiyo sawa |

**Msisitizo**

**Jinsia huingiliana na vigezo vingine kama: umri, tabaka, rangi/kabila, ulemavu, mwelekeo wa kijinsia, kijiografia, kiuchumi, kisiasa na mazingira.**

### 2.2.3 Majukumu ya kijinsia;

Majukumu tofauti kati ya wanawake na wanaume yaliyobainishwa na kuendelezwa kijamii. Mfano, kupika, kufua, kuchota maji na kusafisha nyumba, yanatambuliwa kama majukumu ya kijinsia ya wanawake badala ya kuwa ni majukumu ya wote. Tutofautishe Majukumu ya kijinsia mfano:

i. **Mwanamke:** Kulea na kutunza watoto, walemavu, wagonjwa na wazee ndani ya kaya, kufanya usafi wa nyumbani (kuosha vyombo,kudeki,kufua,kufagia) nk

ii. **Mwanaume:** Kutafuta kipato cha familia, kulinda familia na kuongoza familia

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Inatumika katika kubaini upungufu katika mgawanyo wa majukumu ya kijinsia ambapo mgawanyo huu unakuwa si wa haki na usawa hivyo kumsaidia Afisa wa mipango na bajeti kushughulikia/kuingiza upungufu huo kwenye mipango na bajeti.

### 2.2.4 Mahitaji ya msingi ya jinsia


Ni mahitaji ya jumla na mahsusi yanayotokana na majukumu ya kijamii yanayohusiana na jinsi ya mtu binafsi. Mahitaji haya ni ya vitendo yanayoiwezesha jinsi kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa na jamii husika. Mahitaji haya mara nyingi yanahusishwa na hali halisi ya kila siku ya maisha, kama makazi, maji, kazi, elimu, afya, n.k. na mahitaji haya, yasipotimizwa husababisha kukosekana kwa usawa.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Afisa bajeti azingatie uchambuzi wa mahitaji na vipaumbele katika kuwawezesha wanawake na wanaume kupata mahitaji yao ya msingi ili waweze kushiriki, kufikia, kutumia na kunufaika na fursa na huduma mbalimbali zilizopo.

### 2.2.5 Mahitaji ya kimkakati ya jinsia:

Ni mahitaji yanayohitajika ili kuondoa mifumo, ukatili wa kijinsia na taratibu zinazozuia usawa wa kijinsia na maendeleo jumuishi. Mfano; kuwepo kwa mifumo inayosababisha kukosekana kwa mgawanyo sawa wa majukumu, rasilimali, na fursa za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Afisa bajeti anatakiwa kuzingatia afua zitakazoleta ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika maeneo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Vilevile kuleta mageuzi katika mila na desturi zenye madhara.




### 2.2.6 Takwimu zilizonyumbulishwa kwa Jinsi:

Hizi ni takwimu zilizochambuliwa kwa misingi ya tofauti za kibaiolojia yaani jinsi ya kike na ya kiume.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Takwimu iliyonyumbulishwa kijinsi pekee kwa kawaida huchambuliwa kwa kutumia makundi mawili ya kibaiolojі yaani wanaume na wanawake na kisha hutumika kuandaa mipango na bajeti, mfano utoaji wa huduma na fursa za elimu,afya, maji na n.k. Hata hivyo unyambulishaji wa kibaiolojia si kiwakilishi kizuri cha kijinsia kwasababu haielezei uhusiano wa mamlaka iliyojengwa katika jamii na kanuni za kijinsia zilizopo miongoni mwa wanawake, wanaume na watu wenye ulemavu.

### 2.2.7 Takwimu iliyonyumbulishwa kwa Jinsia:

Ni takwimu zilizochambuliwa kwa misingi ya jinsi, umri, hali ya ulemavu, tofauti za kipato, elimu na maeneo ya kijiografia.

i. **Hii inahitaji maafisa kuhakikisha kuwa kuna ushirikiano wa kisekta/idara/taasisi ili kuweza kupata takwimu sahihi zinazoonyesha hali halisi ya haya makundi ya pembezoni,**

ii. **Inahitaji kupanua wigo wa uelewa ili kuweza kutafsiri zile takwimu ipasavyo na kuweka afua sahihi zinazoweza kubadilisha hali hiyo.**

#### 2.2.7.1 Muingiliano wa makundi mtambuka na Kijinsia/ (intersectionality):

Ni muhimu kuzingatia tofauti za mahitaji ya Kijinsia kulingana na upembuzi yakinifu unaozingatia utofauti uliopo wa mwanaume na mwanamke kulingana na umri, hali ya kuchumi, hali ya kimaumbile na hali ya kimazingira.

**Ufafanuzi wa matumizi dhana hii;** Takwimu hizi hupima tofauti za kijamii na kiuchumi kati ya wanawake na wanaume. Takwimu hizi ni muhimu kwasababu hutuonyesha kama mpango fulani unalenga kunufaisha wanawake, wanaume, wasichana na wavulana katika utofauti wao na kubaini athari tofauti zinazoweza kuleta madhara katika makundi haya.

### 2.2.8 Uchambuzi wa Kijinsia;

Ni upembuzi unaofanyika ili kutambua mahitaji tofauti ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana katika jamii. Vipengele muhimu vya uchambuzi ni mgawanyo wa majukumu, ufikiaji na umiliki wa rasilimali, ufanyaji wa maamuzi na unufaikaji wa fursa na rasilimali zilizowekwa.

Wakati wa uchambuzi wa kijinsia ni muhimu sana kuenda hatua moja zaidi kutafuta kuelewa kwanini hali iko ilivyo ili kubaini kiini cha tatizo na kutengeza afua ambazo zinalenga kuondoa kiini cha tatizo kwa muda mfupi, wa kati na mrefu

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Hii inategemea na eneo/cheo/nafasi uliyopo kama takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tafiti za ajira na kaya (Labour force survey) Sensa ya Watu na Makazi, Takwimu za Kijinsia, SIGI ripoti, Tafiti za Watu na Hali ya Afya, na Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa taasisi husika, Tafiti za tathimini na utafiliaji (M&E report) za taasisi husika, mikakati na programu za taasisi/kisekta.

**Kwa ngazi za mikoa na halmashauri; Tafiti za ziada zinazoweza au zilizofanyika zinaweza kutumika.**

**Msisitizo**


### 2.2.9 Pengo la Kijinsia;


Ni tofauti kubwa au ndogo ya Kijinsia inayoonekana kati ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana unaosababishwa na mfumo usiozingatia usawa wa Kijinsia. Pengo la Kijinsia hujitokeza zaidi kwenye mgawanyo wa majukumu na rasilimali, ufikiaji na umiliki wa rasilimali, ufanyaji wa maamuzi na unufaikaji wa fursa. Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023) imeainisha mapengo ya Kijinsia katika ngazi ya Taifa. Rejea mapengo yaliyoanishwa katika sera.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Kwa kutumia taarifa na nyaraka mbalimbali zilizopo, Afisa bajeti anaweza kubaini na kuweka mipango kulingana na pengo lililopo.

### 2.2.10 Usawa wa Kijinsia na uwiano wa Kijinsia;

Usawa wa kijinsia ni upatikanaji wa haki na fursa sawa za kielimu, kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. Uwiano wa kijinsi ni hali ya mgawanyo wa haki wa rasilimali, fursa, na majukumu kati ya wanaume na wanawake, ili kushughulikia pengo na tofauti zinazotokana na kanuni na matarajio ya kijamii kulingana na jinsia, inalenga kutambua na kushughulikia mahitaji na changamoto za kipekee zinazowakabili watu wa jinsi tofauti. Uwiano wa kijinsia ni mkakati mahsusi wa kufikia usawa wa Kijinsia



#### 2.2.10.1. Dari ya kioo:

Ni hali ambayo kunakuwepo na fursa za maendeleo lakini kundi fulani haliwezi kufikia japo linaziona.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Katika upangaji wa mipango na bajeti ni muhimu afisa kuzingatia kuondoa vikwazo vinavyozuia upatikanaji wa rasilimali na fursa sawa kwa watu wote.

### 2.2.11 Ujumuishaji:

Ni kuondoa vizuizi vinavyozuia ushiriki wa makundi mbalimbali kama vile ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli zote kwa usawa na wengine. Ni kanuni inayowaongoza watu katika kufanya kazi ili kujenga dunia ambayo makundi na jumuiya zote zinaweza kutekeleza haki zao za kibinadamu kikamilifu na bila ubaguzi.

### 2.2.12 Mfumo dume:

Ni dhana inayomuaminisha mwanaume kuwa na nguvu kuliko mwanamke katika nyanja mbalimbali za maisha ikiwemo kisiasa, kiuchumi, maadili na familia. Hali hii, mwanaume anakuzwa na kuaminishwa kuwa hawezi kufikwa na changamoto za Kijinsia. Ni hali ya mfumo wa kijamii inayomfanya mwanaume kuwa na matarajio ambayo yasipofikiwa yanaleta madhara ya kiakili, kisaikolojia hatimae uharibifu wa mahusiano na wengine.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Ni muhimu upangaji wa bajeti uzingatie hali halisi kulingana na  mahitaji ya msingi na kimkakati ya wanaume na wavulana (Mwasilishaji atoe mfano wa sekta ambayo hali hii inajitokeza zaidi).

### 2.2.13 Mila, tamaduni na desturi  za Kijinsia:

Ni matarajio au mitazamo ya kijamii inayomtambulisha mwanamke au mwanaume iliyojengeka na kukubalika katika jamii. Mfano, mwanaume anatarajiwa kuwa kiongozi, baba wa familia, mkuu wa kaya, mfanyabiashara mkubwa, mwenye mamlaka wakati mwanamke anatarajiwa kuwa mtiifu, aolewe, mrembo, awe mpole, alee familia, awe tegemezi kwa jamii.

**Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii;** Ni muhimu mipango na bajeti iangalie vikwazo vinavyotokana na mila na desturi katika jamiii/sekta na  taasisi husika ili kuleta usawa wa Kijinsi

### 2.2.14 Programu za kuleta mabadiliko ya usawa wa Kijinsia:

Hizi ni shughuli/afua zinazotekelezwa ili kuondoa vikwazo vya kimfumo na kuimarisha usawa wa Kijinsia katika jamii/sekta/taasisi.

**Mfano 1:** Programu ya Viti Maalumu katika nafasi za uwakilishi kama vile Ubunge ; Mfano 2: Program maalumu kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa wasichana katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu

Ufafanuzi wa matumizi ya dhana hii; Programu hizi zinalenga kuleta mabadiliko chanya na kubadili mitazamo na tabia zisizokuwa na usawa kwenye jamii kwa kuwawezesha wanawake na wasichana, kuwashirikisha wanaume na wavulana na kuhusisha taasisi na Serikali katika kupinga vitendo vya kibaguzi na kukuza fursa na usawa kwa watu wote katika jamii.

### 2.2.15 Mazoezi Sura ya Pili

Mwezeshaji atumie kati ya mazoezi haya kulingana na aina ya washiriki alionao.

**Zoezi la kwanza**

i. Washiriki watagawanyika katika vikundi vidogo vya watu watano mpaka nane. Kila kundi litapewa jozi yenye dhana mbalimbali na maelezo yenye ufafanuzi kwa ajili ya kuzihusianisha.

ii. Kila kikundi kijadili maelezo yaliyotolewa na kutafuta dhana sahihi inayoendana na maelezo hayo

iii. Kikundi kitawasilisha majibu yao

**Zoezi la pili**

Tumia picha kutofautisha majukumu ya kijinsi na kijinsia na kijamii kati ya wanawake/ wasichana na wanaume/wavulana

i. Kundi la kwanza-majukumu ya kijinsi

ii. Kundi la pili-majukumu ya kijinsia

iii. Kundi la tatu-majukumu ya kijamii

Washiriki vilevile waeleze ni kwa jinsi gani mgawanyo huo wa majukumu unavyoathiri kwa namna tofauti tofauti wanawake/wasichana na wanaume/ wavulana, na inamaana gani kwenye mgawanyo wa rasilimali

**Zoezi la tatu**

Katika vikundi ,washiriki waainishe mahitaji ya kimkakati na ya kawaida ya,

i. Watoto wa kike na wa kiume wa rika balehe (kundi la kwanza);

ii. Watoto wenye ulemavu (zingatia aina mbalimbali za ulemavu) walioko kwenye rika balehe (kundi la pili)

iii. Wanafunzi wa vijijini na wanafunzi wa mijini

Katika mahitaji ya mkakati na ya msingi ainisha; Watoto wa kike na kiume; Umri- zingatia makundi yote ya rika ; Elimu; Afya; Maji; Miundombinu na n.k

# 3. SURA YA TATU - UKONDOISHAJI WA MASUALA YA KIJINSIA KATIKA MIPANGO NA BAJETI

Sura hii itakuwa na sehemu mbili, ya kwanza itaelezea uelewa na mbinu na dhana mbalimbali za bajeti na ukondoishaji wa usawa wa Kijinsi katika sera, mikakati na mipango (Gender mainstreaming). Aidha sehemu ya pili itazungumzia uelewa na mbinu za upangaji wa mipango na bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

## 3.1 MAANA YA NENO BAJETI NA DHANA MBALIMBALI ZA BAJETI

### 3.1.1 Bajeti

Ni mpango wa kifedha unaoonyesha makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi fulani kawaida mwaka mmoja. Inasaidia kupanga, kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali ili kufikia malengo fulani. Bajeti hutumika katika ngazi mbalimbali kama familia, mashirika au Serikali.

### 3.1.2 Bajeti ya Serikali;

Ni mpango unaoonesha namna Serikali itakavyokusanya na kutumia fedha katika kipindi cha mwaka mmoja kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi. Kupitia bajeti, Serikali inapanga kutumia mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali yatakayokusanywa kwa ajili ya kugharamia utoaji wa huduma kwa wananchi kama vile elimu, afya, maji na barabara.

### 3.1.3 Bajeti yenye mrengo wa kijinsia;

Ni bajeti ambayo inazingatia masuala yote yanayohusiana na jinsia, na inatambua na kuzingatia masuala hayo katika mipango na sera za matumizi ya afua mbalimbali. Ni bajeti ambayo inahusisha makundi yote (wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, watu wenye mahitaji maalumu) kwa kuhakikisha upangaji na ugawaji wa rasilimali wenye usawa wa kijinsia, kwa kuchangia au kuwezesha usawa katika ufikiaji wa fursa sawa kwa wote. Ni mgawanyo wa rasilimali unaojumuisha uchambuzi wa mapato na matumizi kwa mtazamo unaozingatia usawa na uwiano wa kijinsia. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa bajeti inayozingatia mahitaji ya kijinsia yatakuwa na manufaa sawa kwa makundi yote.

***Bajeti yenye mrengo wa kijinsia*** ni mchakato wa kupanga, kutenga, kutumia, na kufuatilia bajeti kwa kuzingatia mahitaji, hali, na athari tofauti kwa wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, na makundi mengine (watoto, wazee, wajane, watu wenye ulemavu). Husaidia kuhakikisha kwamba rasilimali fedha zinagawanywa na kutumika kwa njia inayozingatia usawa wa kijinsia, ili kila mtu awe mwanaume au mwanamke anufaike kwa haki.

### 3.1.4 Bajeti yenye msisitizo wa Jinsia;

Inaonyesha ufahamu wa jinsia na inamaanisha kuwa sera ya bajeti au programu inatambua athari muhimu za destruri za kijinsia, majukumu na mahusiano.

### 3.1.5 Bajeti Isiyofungamana na Jinsia;

Ni bajeti ambayo ukusanyaji wa mapato, matumizi ya Serikali na sera za fedha huandaliwa na kutekelezwa bila kuzingatia kwa njia yoyote mahitaji mahsusi ya kijinsia, tofauti au athari. Kwa maneno mengine, haizingatii mahitaji na uzoefu tofauti wa wanawake, wanaume, na makundi mbalimbali ya jamii.

### 3.1.6 Bajeti Kipofu/Isiyoona Jinsia;

Mipango na bajeti zisizozingatia jinsia zinawachukulia watu katika jamii kama watu wa jinsi moja, wakipuuza majukumu tofauti, wajibu, uwezo, mahitaji na vipaumbele vya wanawake na wanaume.

## 3.2 UMUHIMU WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA

i. **Kushughulikia Ukosefu wa Usawa wa Kijinsia:** Bajeti yenye mrengo wa kijinsia inatambua kwamba bajeti za Serikali zina athari tofauti kwa wanaume na wanawake kutokana na tofauti zilizopo za kijinsia. Kwa kuchanganua mgao wa bajeti kwa mtazamo wa kijinsia, watunga sera wanaweza kutambua na kurekebisha ukosefu wa usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa rasilimali, huduma, na fursa sawa.

ii. **Kukuza uwezeshaji wa Wanawake na makundi mbalimbali katika jamii yaliyoachwa nyuma:** Bajeti yenye mrengo wa kijinsia inalenga kuboresha upatikanaji wa rasilimali za kiuchumi, elimu, huduma za afya, na huduma nyingine muhimu kwa wanawake na wasichana. Kwa kutilia mkazo ufadhili wa mipango na miradi inayounga mkono uwezeshaji wa wanawake, hii inaweza kusaidia kuondoa vikwazo vya ushiriki wa wanawake, watu wenye ulemavu na watoto katika uchumi na jamii.

iii. **Kuboresha Utoaji wa Huduma:** Kutengeneza bajeti zenye mrengo wa kijinsia kutasaidia Serikali kugawa rasilimali kwa ufanisi zaidi ili kukidhi mahitaji maalum ya wanawake na wasichana, wanaume na wavulana na watu wenye mahitaji maalumu. Hii inaweza kujumuisha ufadhili wa elimu na huduma za afya ya uzazi kwa vijana, pamoja na kushughulikia unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.

iv. **Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi:** Bajeti zinazozingatia jinsia zinakuza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma kwa kufanya mchakato wa bajeti kuwa shirikishi zaidi. Kwa kushirikisha vikundi vya wanawake na mashirika ya kiraia katika uandaaji na ufuatiliaji wa bajeti, hii inasaidia kuhakikisha kuwa rasilimali za Serikali zinatumika kwa ufanisi na usawa kwa wote.

v. **Kuboresha malengo ya ukuaji wa uchumi:** Bajeti yenye mrengo wa kijinsia ni muhimu katika kuendeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususani Lengo namba tano (5) juu ya usawa wa kijinsia na Lengo namba moja (1) la kutokomeza umasikini. Kwa kuzingatia masuala ya kijinsia katika sera, mipango na bajeti, Serikali itaweza

kuchangia kufanikisha ajenda ya maendeleo jumuishi na endelevu.

vi. **Kukuza Ukuaji wa uchumi:** Usawa wa kijinsia sio tu suala la haki za binadamu bali pia ni hitaji la kiuchumi. Utafiti umeonyesha kuwa kukuza usawa wa kijinsia kunaweza kusababisha uzalishaji mkubwa zaidi, ukuaji wa Pato la Taifa, na kupungua kwa umasikini. Bajeti yenye mrengo wa kijinsia itasaidia kutoa fursa kwa wanawake kama wachangiaji katika ukuaji wa uchumi na maendeleo. Bajeti yenye mrengo wa kijinsia ni muhimu katika kuleta usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa wanawake, na maendeleo jumuishi. Kwa kuzingatia masuala ya kijinsia katika sera na upangaji wa bajeti, Serikali inaweza kuleta usawa wa kijinsia na fursa sawa katika jamii.

## 3.3 KANUNI ZA UPANGAJI WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA

Upangaji wa bajeti inayolenga Jinsia lazima uongozwe na kanuni za msingi ambazo huleta ufanisi kwenye utekelezaji wake . Kanuni hizi zinatoa mwongozo wa kuhusisha masuala yote ya kijinsia katika hatua zote za mchakato wa bajeti na kuendeleza usawa wa kijinsia. Kanuni hizi ni pamoja na:

i. **Usawa wa Kijinsia:** Maamuzi ya bajeti yanapaswa kusaidia kupunguza tofauti za kijinsia na kukuza fursa sawa kwa makundi yote kwa kutenga rasilimali kwa kuzingatia usawa.

ii. **Kutokuwepo kwa Ubaguzi:** Bajeti ilenge kuondoa ubaguzi na upendeleo wa kijinsia katika mgao wa rasilimali na sera. Isisitize haki ya kila mtu kupata huduma za kijamii kwa usawa.

iii. **Uchambuzi wa Kijinsia:** Uchambuzi wa kijinsia ni msingi wa bajeti, ukihusisha tathimini ya kimfumo ya jinsi maamuzi ya bajeti yanavyoathiri makundi tofauti ya kijinsia. Uchambuzi huu husaidia kubaini tofauti zilizopo na mahitaji maalum ya wanawake, wasichana, wanaume, wavulana, pamoja na watu wenye mahitaji maalumu. Kabla ya kutenga fedha, tathmini ifanyike kuhusu mahitaji tofauti ya wanawake/wasichana na wanaume/wavulana katika sekta mbalimbali kama afya, elimu, kilimo n.k.

iv. **Husisha:** Bajeti yenye mrengo wa kijinsia si mchakato wa kipekee bali unaingizwa katika hatua zote za mzunguko wa bajeti, kuanzia uundaji na utekelezaji hadi ufuatiliaji na tathmini. Hii inahakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanaingizwa katika maamuzi yote yanayohusiana na bajeti.

v. **Malengo ya kijinsia na shabaha:** Bajeti zinazoandaliwa zizingatie malengo na shabaha zinazohusiana na usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa wanawake na kupunguza tofauti za kijinsia. Malengo haya yaongoze mgao wa rasilimali na uundaji wa sera ulio na usawa.

vi. **Ushiriki na Ushirikishwaji:** inasisitizwa kuwe na ushiriki wa wanawake, wasichana, wanaume, wavulana na makundi ya kijinsia yaliyotengwa katika michakato ya kufanya maamuzi kuhusu bajeti. Wanawake na wanaume, na makundi ya kijinsia yaliyo pembezoni, washirikishwe kikamilifu katika kupanga na kuamua bajeti.

vii. **Mgawanyo wa Rasilimali:** Fedha zitengwe kulingana na uhalisia wa changamoto za kijinsia zilizobainishwa kupitia takwimu na utafiti.

viii. **Uwazi na Uwajibikaji:** Serikali na taasisi ziwe wazi juu ya jinsi bajeti inavyotumika na iwajibike kwa kutoa matokeo ya kijinsia kwa wananchi.

ix. **Ufuatiliaji na Tathmini:** Kupima kama matumizi ya bajeti yameleta mabadiliko chanya kwa usawa wa kijinsia, na kufanya marekebisho inapohitajika.

x. **Utetezi na Uwekezaji katika Kujenga Uelewa na Ujuzi wa GRB:** Kukuza uelewa na utetezi wa upangaji wa bajeti unaozingatia jinsia ni muhimu. Hii inajumuisha juhudi za kujenga uungwaji mkono miongoni mwa watunga sera, mashirika ya kiraia, na umma kwa ujumla ili kuingiza masuala ya kijinsia katika bajeti.

xi. **Kuweka mipango ya muda mrefu:** Ili kufikia usawa wa kijinsia upangaji wa bajeti ni suala la muda mrefu na linalohitaji juhudi. Hii itasaidia kuleta mabadiliko endelevu na kuhakikisha kuwa masuala ya kijinsia ni sehemu muhimu ya taratibu za bajeti.

**Zoezi la nne**

**Majadiliano ya kikundi kuhusu kanuni za Bajeti yenye mrengo wa kijinsia,Wagawanye washiriki katika vikundi vidogo vya washiriki watano mpaka nane.**

i. Kila kikundi kitapewa kanuni moja au mbili za Bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

ii. Kila kikundi kijadili uelewa wao wa kanuni hizo na kutoa mifano ya jinsi inavyoweza kutumika katika kupanga bajeti.

iii. Kila kikundi kiwasilishe majibu yake mbele ya wengine.

## 3.4 HATUA KWA HATUA KATIKA UANDAAJI WA BAJETI YENYE MRENGO WA KIJINSIA.

### 3.4.1 HATUA YA 1: Kutathmini mazingira wezeshi ya usawa wa Kijinsia

**Lengo:**

i. Kuainisha malengo na matamko ya sera yenye mrengo wa kijinsia

ii. Kuainisha afua au maeneo ya kipaumbele kutoka kwenye mikakati ya sera zenye mrengo wa kijinsia

iii. Kuainisha viashiria vya kijinsia (gender indicators) vilivyoko katika mikakati ya sera pamoja na viashiria vilivyoko katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDPs)

iv. Kutambua sheria zinazo unga mkono jitihada

**Mazingira wezeshi** ni hali ambayo inajumuisha mifumo, sera za taifa zilizopo, sera za kitaasisi, miongozo, sheria zinazoelekeza uandaaji wa mipango na bajeti kwa mrengo wa Kijinsia. Mazingira wezeshi ni pamoja na maazimio na makubaliano ya Kimataifa, Kikanda, Kitaifa na miundo ya kimfumo inayohusiana na kutegemeana, ili kuwezesha kukuza usawa wa kijinsia.

## Zoezi la tano

Fanya tathmini ya mapitio ya sera, mipango, mikakati na mapitio ya mwaka wa utekelezaji , katika sekta/ taasisi, mkoa na halmashauri husika . Kila mshiriki atafanya mapitio ya mipango na bajeti zao ili kuangalia ukondoishaji wa masuala ya kijinsia katika bajeti kwa kila mwaka na kutambua masuala yaliyo ainishwa pamoja na changamoto katika idara au taasisi husika na kubainisha fursa na vikwazo vya usawa wa kijinsia.

Washiriki watawasilisha matokeo ya mipango na bajeti zao ili kubaini mapungufu na fursa zilizopo katika ukondoishaja wa masuala ya kijinsia katika bajeti kwenye taasisi zao. ( Elimu, Afya, Miundombinu, Maji, Mazingira n.k).

## Zoezi la sita

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, ilifanya ufuatiliaji na tathmini (M&E) ya madawati ya jinsia 150 katika taasisi za elimu ya kati na ya juu pamoja na masoko ya umma. Ripoti inaonesha kuwa madawati ya jinsia yanatoa huduma za kuzuia na kupinga ukatili wa kijinsia (GBV) kwa wanafunzi na wanajamii wengine. Hata hivyo, huduma hizi zingeweza kuwa bora zaidi kama taasisi hizi zingetenga bajeti mahsusi kwa ajili ya madawati ya jinsia.

i. Ni masuala gani ya kijinsia ambayo yanapaswa kufanyiwa ukondoishaji katika mipango na bajeti ya taasisi hizo?

ii. Ni taasisi zipi za Serikali zinapaswa kufanya ukondoishaji wa bajeti za madawati ya jinsia katika mipango yao?

## Zoezi la saba

Lengo kuu la Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ni kuhakikisha kunakuwepo na usawa wa kijinsia katika jamii kwa ujumla. Ili kufanikisha hili, sera inatilia mkazo maeneo yafuatayo:

i. Kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi kwa kuwapatia fursa sawa za kupata kipato na ajira zenye tija, ili kuboresha hali zao za maisha na kupunguza utegemezi wa kiuchumi.

ii. Kupambana na kuondoa kabisa aina zote za ukatili wa kijinsia,

iii. Kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi na ngazi mbalimbali za maamuzi.

Ni matarajio ya Serikali kwamba kila sekta au taasisi ya umma na binafsi itaangalia malengo haya na kuyatafsiri kwa vitendo kulingana na changamoto, fursa, na mazingira ya sekta husika. Hii itahakikisha kuwa juhudi za kuleta usawa wa kijinsia zinafanyika kwa njia jumuishi na endelevu katika nyanja zote za maendeleo.

Tumia jedwali hapo chini kama mfano kuainisha changamoto zinazowapata wasichana katika sekta yako;

| Changamoto zinazowapata wasichana kupata haki ya elimu | Nini kifanyike kutatua hili | Kuna kifungu cha bajeti? | Bajeti tayari imetengwa kwa kazi hii? Kama ndio ni kiasi gani?na je inatosha? | Kama hakuna bajeti, hii inawezaje kuweka katika mpango na wapi? | Ni kiasi gani kinahitaji kutengwa | Kuna idara nyingine zimetenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vyoo? | Nani anatakiwa kuhusishwa katika mchakato wa bajeti katika ujenzi huu? | Elezea hatua zitakazo fuata ili kuhakikisha ujenzi huu unabajetiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfano: Ukosefu wa vyoo shuleni vilivyotengwa kwa jinsi | Ujenzi wa vyoo vipya | Ndio Kifungu namba 507 | Ndio lakini kwa ujenzi wa matundu ambayo pia hayatoshi | Vyoo vinatakiwa kuwa na ubora wa juu, vilivyotengwa kwa jinsi na vianyozingatia Watoto wenye mahitaji maalum | Tumia bajeti yoyote kama mfano | Bajeti kuu ya Wizara ya Elimu? | Shule, Kata ambapo vyoo vitajengwa | Weka vigezo vya ujenzi na gharama pia shirikisha watu kwenye kata |

**Kisa Mafunzo: Mipango wa Matumizi wa Nusu mwaka Kigoma na Geita**

| **Matokeo ya Rubriki kutoka kwenye Utafiti wa GRB wa Mradi wa KAGIS (2023) : Plan International** | | | |
|---|---|---|---|
| Enao la Tathmnini | Alama 1-3 (1 chini, 3 juu) | | Maoni |
| | Kigoma | Geita | |

| Matokeo ya Rubriki kutoka kwenye Utafiti wa GRB wa Mradi wa KAGIS (2023) : Plan International | | | |
|---|---|---|---|
| Uzingatiaji wa Sera na ahadi za Kitaifa zenye matamko ya kijinsia | 1.15 | 0.89 | Mipango na bajeti za wilaya zinalingana na sehemu ndogo ya ahadi za ngazi ya kitaifa na mahitaji yanayoongoza usawa wa kijinsia na ushirikishwaji. |
| Utambuzi wa usawa wa kijinsia na masuala ya haki za wasichana ambayo yanahitaji kujumuishwa katika mipango ya Wilaya | 0.66 | 0.45 | Kuna kiwango cha chini cha utambuzi, kuzingatia na kujumuisha usawa wa kijinsia na masuala ya haki za wasichana katika mipango ya wilaya, na utekelezaji wake. |
| Ufanyikaji wa uchambuzi na Usawa wa Jinsia | 0.81 | 1.24 | Kuna ushahidi mdogo wa tathmini yoyote rasmi ya usawa wa kijinsia inayotumiwa na Halmashauri wakati wa kupanga na kupanga bajeti. |
| Hatua zinazochukuliwa kushughulikia usawa wa kijinsia na masuala ya haki za wasichana | 1.65 | 1.14 | Hatua ndogo zilichukuliwa kushughulikia usawa wa kijinsia na haki za wasichana. |

### 3.4.2 HATUA YA 2: Kutathmini mazingira wezeshi ya usawa wa Kijinsia

**Lengo:**

i. Kukusanya takwimu zilizonyambulishwa kwa jinsi na jinsia

ii. Kuainisha mapengo ya kijinsi na kijinsia kutoka kwenye data/takwimu/taarifa au kuainisha changamoto za kijinsi/kijinsia (Ushirikishwaji/Ushiriki wa Wadau huanza kujitokeza katika hatua hii)

iii. Kufanya uchambuzi wa kina wa visababishi (wazi-binafsi, ndani-jamii taasisi, kina sera sheria na miongozo)

iv. Kubuni afua/programu stahiki za kukabiliana, visababishi na kuziba pengo lililoainishwa

v. Kuweka malengo ya kijinsia katika mipango na bajeti

vi. Weka viashiria vya matokeo (Progress and Outcome Indicators) katika kila lengo

Kuweka malengo ya kijinsia katika mipango na bajeti ni hatua muhimu sana katika kuleta usawa kijinsia. Hatua hii inahakikisha kwamba usawa wa kijinsia unakuwa unakondoishwa katika mipango na bajeti. Katika hatua hii

i. Tumia mwongozo wa bajeti unaotoa maelekezo ya ukondoishaji wa masuala ya kijinsia katika maandalizi ya bajeti

ii. Hakikisha mipango ya bajeti na sera inajumuisha Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), pamoja na Mpango wa Kitaifa wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (NPAVAWC II 2024/25 – 2028/29)

iii. Jumuisha viashiria vya jinsia na shabaha zilizopo katika mpango kazi wa kila sekta

iv. Shawishi na tenga bajeti kwa ajili ya afua mahsusi za kijinsia

v. Husisha wadau mbalimbali muhimu, kama vile vikundi vya wanawake, mashirika yanayotetea haki za wanawake na Kikosi kazi cha kuhuisha masuala ya kijinsia katika sera za kisekta ili kufadhili na kutanua wigo.

**Zoezi la nane**

Mradi wa ujenzi wa barabara mpya ya mtaa.

i. Kwenye mchakato wa kujenga barabara nani ni muathirika zaidi katika jamii?

ii. Nani ni mnufaika mkuu katika ujenzi wa barabara hii?

iii. Je makundi mbalimbali katika jamii yalishirikishwa katika mpango wa ujenzi wa barabara hii?

iv. Je, maeneo ya barabara ni salama kwa wanawake na makundi mengine hasa nyakati za usiku?

v. Je, barabara inaunganisha huduma mbalimbali za kijamii kama hospitali, shule au soko?

## Zoezi la tisa

Halmashauri ya mji inapanga bajeti ya mwaka wa 2025 kwa sekta ya elimu. Kuna jumla ya Tsh milioni 100 za kutenga. Mahitaji ni:

| Mahitaji | Gharama | Maelezo ya Kijinsia |
|---|---|---|
| Ukarabati wa vyoo vya shule | 20M | Vyoo vya wasichana ni vichache na vibovu |
| Ununuzi wa madawati | 15M | Watoto wote wana shida ya madawati |
| Mafunzo ya walimu kuhusu jinsia na ukatili | 10M | Walimu hawana uelewa kuhusu usawa wa kijinsia |
| Ujenzi wa bweni la wasichana | 40M | Wasichana huacha shule kwa sababu ya umbali |
| Kununua kompyuta za shule | 15M | Shule haina mafunzo ya TEHAMA kwa wote |

**Jukumu la Vikundi:**

i. Gawanya washiriki katika vikundi.

ii. Kila kundi litengeneze bajeti kwa kutumia hiyo Tsh 100M.

iii. Washirikishe mtazamo wa kijinsia: nani anafaidika? nani atapuuzwa?

iv. Andaa majibu kama jedwali na uwasilishe.

## Zoezi la kumi

**Maswali ya kuchochea mjadala:**

Je, bajeti yenu imezingatia mahitaji ya jinsi zote?

Je, kuna matumizi ambayo yangeongeza usawa wa kijinsia?

Nini kingeweza kubadilishwa ili kuwajumuisha zaidi wasichana/wavulana/watu wenye ulemavu?

### 3.4.3 HATUA YA 3: Kutathmini uwezo wa kitaasisi wa kutekeleza mipango na bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Mambo ya kuangalia katika mfumo na taratibu za Kitaasisi yanayoweza kusaidia upatikanaji sawa na bora wa huduma za kijamii kwa Wanawake na Wasichana, wavulana na wanaume na watu wenye mahitaji maalum na kuleta Usawa wa Kijinsia. Hii ni pamoja na: -

i. Uwepo wa uelewa wa Masuala ya Jinsia ndani ya taasisi

ii. Mfumo wa uwajibikaji wa pamoja katika masuala ya usawa wa kijinsia

iii. Ushiriki Sawa wa Wanawake na Wanaume katika Miundo ya Uongozi wa Taasisi

iv. Utashi na Utayari wa Viongozi wa Ngazi za Juu katika masuala ya Usawa wa Jinsia

v. Kutambua majukumu na wajibu wa kila mdau

vi. Uwepo wa Rasilimali za Kifedha kwa ajili ya afua za Usawa wa Jinsia.

**Zoezi la kumi na moja**

Wagawe washiriki kutoka taasisi au sekta moja katika vikundi vidogo na wajadiri maswali yafuatayo:

i. Ni maafisa wangapi katika idara yako walipata mafunzo ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia?

ii. Je, taasisi ina kitabu chochote au mwongozo wa jinsia ambao hutumika wakati wa kuandaa mpango na bajeti?

iii. Je, taasisi yako ina orodha ya ukaguzi inayoonyesha masuala ya kipaumbele ya kushughulikiwa ili kuhakikisha wanawake na wasichana, wanaume na wavulana wanapata huduma zinazozingatia jinsia?

iv. Je, kuna utaratibu rasmi wa kufundisha wafanyakazi wapya wanaokuja kuhusu bajeti yenye mrengo wa kijinsia ili kuziba mapengo yaliyoachwa kwa sababu ya mabadiliko?

v. Je, ni nani anaehusika kuhakikisha kwamba bajeti imezingatia masuala ya kijinsia kwenye taasisi yako?

vi. Je, mnaona ni maeneo gani katika taasisi bado hayazingatii usawa wa kijinsia na yanahitaji bajeti mahsusi?

Kila kikundi kishirikishe mipango yao ya kushughulikia changamoto za ndani katika kutekeleza au kupanga bajeti yenye mrengo wa kijinsia kwa mwaka ujao.

### 3.4.4 HATUA YA 4: Ushiriki na Ushirikishwaji wa wadau mbalimbali

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 inatambua kuwa utekelezaji wa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake (GEWE) ni jukumu la pamoja kwa sekta zote wizara za Serikali, wadau wa sekta binafsi, na mashirika yasiyo ya kiserikali. Sera hii inasisitiza mbinu jumuishi na shirikishi katika utekelezaji wake, ambapo uratibu wa kisekta na wa sekta mbalimbali ni msingi muhimu wa kufanikisha malengo yake.

Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya uratibu wa masuala ya kijinsia kwa kuhusisha taasisi mbalimbali katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unajumuishwa kikamilifu katika mipango, sera na bajeti. Baadhi ya taasisi zinazopaswa kusimamia na kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya kijinsia ni pamoja na:

i. **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**, ambayo ndiyo wizara yenye dhamana ya kusimamia uratibu wa sera za jinsia kitaifa na utoaji wa msaada wa kitaalamu na hivyo inapaswa kuongoza ukondoishaji wa masuala ya kijinsia katika taasisi zote za umma na binafsi.

ii. **Wizara ya Fedha** inawajibika kuhakikisha kuwa bajeti za sekta zote zinajumuisha masuala ya kijinsia, ikiwemo kutenga rasilimali kwa ajili ya kuimarisha usawa wa kijinsia.

iii. **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia** yenye dhamana ya kusimamia vyuo vikuu, vyuo vya kati na taasisi za mafunzo, inapaswa kuhakikisha kuwa usawa wa kijinsia unajumuishwa katika miongozo ya upangaji wa bajeti, usimamizi na ufadhili wa taasisi hizo.

iv. **Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI** ina nafasi muhimu katika kuwezesha uanzishaji na uendelezaji wa masuala ya kijinsia katika maeneo yote ya utekelezaji wake na kuhakikisha kuwa Serikali za mitaa zinakondoisha masuala ya kijinsia kwenye mipango yao ya maendeleo na bajeti za halmashauri.

v. **Wizara ya Viwanda na Biashara** pamoja na **mamlaka za Serikali za Mitaa** zinapaswa kuhakikisha kuwa usawa wa kijinsia unakondoishwa katika masoko na kutengewa bajeti mahsusi na kuungwa mkono kupitia programu za uendelezaji biashara na uwezeshaji kiuchumi.

vi. **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)** na **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET)** kama mamlaka za udhibiti wa elimu ya juu na ya kati, zihakikishe kuwa mahitaji ya usawa wa kijinsia yamejumuishwa katika vigezo vya usajili, ithibati na miongozo ya uendeshaji wa taasisi zinazozisimamia.

**Mchakato wa Maandalizi ya Bajeti na Ushirikishwaji wa Wadau**

| Mzunguko wa bajeti ya Serikali | | | |
|---|---|---|---|
| TAREHE | SHUGHULI | TAASISI HUSIKA | FURSA ZILIZOPO |
| Jul 01 – Jun30 | Huu ni mwaka wa fedha wa kiutekelezaji | Wadau wote wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na Serikali na wanajamii | Usambazaji wa tafiti, machapisho, mapitio na uchambuzi wa bajeti mbalimbali zinazozingatia jinsia na utekelezaji wake |
| August - September | Maandalizi ya mwaka ujao wa fedha. Halmashauri za Wilaya kuwasilisha mwongozo wa mchakato wa utambuzi wa vipaumbele vya jamii na maoni ya miradi ya maendeleo kwa viongozi wa mitaa ngazi ya kijiji/mitaa/kata. MAANDALIZI YA MWONGOZO WA BAJETI YA TAIFA | Halmashauri za Wilaya, WDC/ Kijiji/ mtaa Kamati ya Bajeti, DPPs, makatibu wakuu n.k | -mafunzo kwa CMT, WDC, WEOs, VEOs, na Madiwani kuhusu maandalizi ya bajeti ya jumla Kukutana na Wajumbe wa Bodi na Kamati ya Bajeti katika ngazi ya Taifa, OW-TAMISEMI, na wadau wengine wa bajeti. NGOs zina fursa ya kushirikiana na Serikali katika eneo hili |
| October | Mikutano ya robo ya pili ya mwaka ya kupitisha vipaumbele vya wananchi na maoni ya miradi ya maendeleo katika kila ngazi ya kijiji/mitaa. | VEOs na wananchi | Wadau wa maendeleo kuchangamkia fursa ya kuimarisha uwezo wa jamii kutumia lenzi za jinsia wakati wa kubainisha masuala ya jinsia katika maeneo yao. |
| November - December | Viongozi wa mitaa kwa kushirikiana na Halmashauri kuwasilisha mipango shirikishi ya Mtaa au kijiji (Mipango ya wananchi) kuhusu (O&OD) kwenye halmashauri za wilaya husika kwa ajili ya mapitio. | WDC/WEO | Mafunzo kwa madiwani ili kuwawezesha kupokea mipango ya wilaya, CMT inaweza kuimarishwa kwa kutumia uchambuzi wa awali wa kijinsia wa bajeti za wilaya na mapungufu ya kijinsia yaliyotambuliwa |

| Mzunguko wa bajeti ya Serikali | | | |
|---|---|---|---|
| December | WDC kukutana kwa ajili ya kupitisha na kuandaa mipango ya bajeti ya kijiji/mitaa ya kata zote kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye halmashauri husika. | WDC/WEO | Wanajamii lazima waimarishwe ili kuwa na ajenda zao za bajeti na mapendekezo yatakayowasilishwa katika ngazi ya kata. AZAKi lazima zihakikishe ushiriki katika mikutano ya WDC ikiwa hawajaalikwa, lazima waulize WEO nia yao ya kuhudhuria |
| January | Mipango ya bajeti ya kata kupitishwa katika ngazi ya wilaya na makusanyo kwa ajili ya kuanzisha bajeti ya wilaya moja | CMTs pamoja na kamati ya bajeti ya wilaya | Kutoa mafunzo kwa CMT kwa kuangalia masuala mbalimbali ambayo yalijumuishwa wakati wa kuandaa bajeti |
| February | Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na halmashauri kupitia na kupitisha bajeti ya halmashauri ya wilaya | DCC/RCC/Kamati ya Kudumu ya Madiwani, Wadau Wengine | Asasi za kiraia zinaalikwa kushiriki katika mkutano huo, pamoja na ajenda zao na kuishauri Serikali kuzingatia usawa wa kijinsia katika bajeti. |
| | Kupitia na kurekebisha bajeti ya baraza ambayo iliidhinishwa na Baraza Kamili, DCC, RCC | TAMISEMI, Idara ya Bajeti za Serikali za Mitaa | Endelea kufanyia kazi idara ya bajeti ya Serikali za Mitaa |
| March | Mapitio ya Bajeti ya Halmashauri, mchango wa takwimu na uchapishaji wa vitabu vya bajeti (Kamati ndogo ya Bajeti ya Serikali kuu inakutana) | Wizara ya Fedha, Utumishi wa Umma, TAMISEMI | Kuhamasisha kamati za bunge kuhusu masuala ya msingi ya jinsia ziwe tayari kuchambua bajeti kwa mtazamo wa kijinsia. |
| April- June | Mjadala wa kina wa bajeti zote za sekta na bajeti ya taifa katika kamati za Bunge na Bunge hupitisha bajeti husika. | Bunge na wataalum kutoka wizara za kisekta | Shiriki, fuata majadiliano, na utoe ushauri zaidi wa kiufundi |

Tengeneza orodha kamili ya wadau na makundi ya wadau wanaopaswa kushirikishwa katika michakato ya upangaji, utekelezaji na tathmini ya bajeti. Tafakari ni kwa kiasi gani makundi haya ya wadau yameshirikishwa katika kila hatua muhimu ya mchakato wa upangaji wa bajeti hadi sasa. Baadae, jadili maswali yafuatayo:

i. Nini kinaweza kuzingatiwa wakati wa ushirikishwaji wa wadau mbalimbali, wakiwemo wasichana na wanawake, katika mchakato wa kupanga bajeti za kisekta?

ii. Ni mapendekezo gani yanaweza kutolewa ili kuboresha upangaji wa bajeti na mchakato wa tathmini ili kuhakikisha kwamba vipaumbele vinaakisi mahitaji tofauti ya wanawake na wasichana na wanaume na wavulana, na kuhakikisha ushiriki wa wa vikundi na watu binafsi?

iii. Nini kifanyike ili kukabiliana na mapungufu katika ushirikiano na wadau katika mchakato ujao wa kupanga bajeti?

### 3.4.5 HATUA YA 5: Kuandaa mpando ( wa muda mfupi na wakati) na kutenga bajeti kwenye afua/program za usawa wa Kijinsia

**Mambo ya kuzingatia wakati wa ukondoishaji na Upangaji wa bajeti ya masuala ya kijinsia.**

i. Tenga rasilimali kwa programu na huduma mahsusi ambazo zinalenga kuondoa tofauti za kijinsia zilizobainishwa wakati wa uchambuzi wa kijinsia.

ii. Kagua na kutathmini vipengele vyote vya bajeti ili kuhakikisha kuwa havichangii bila kukusudia kukosekana kwa usawa wa kijinsia.

iii. Zingatia dhana ya uwiano wa kijinsia wakati wa kugawa rasilimali

iv. Tathmini athari za kila matumizi kwa jinsi tofauti na urekebishe mgao ipasavyo

### 3.4.6 HATUA YA 6: Utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini zinazozingatia jinsia.

Katika kuzingatia ukondoishaji wa masuala ya kijinsia katika bajeti za kisekta na taasisi, mwezeshaji anatakiwa kuzingatia vipengele muhimu vifuatavyo:

i. Andaa Viashiria vyenye mrengo wa kijinsia: Andaa viashiria vya kijinsia vilivyo wazi na vinavyoonyesha malengo ya bajeti. Viashiria hivi vinapaswa kuonesha tofauti za kijinsia, uwezeshaji wa wanawake na wanaume, na athari za mgao wa bajeti kwa makundi.

ii. Panga takwimu kulingana na jinsia: Kusanya na chambua takwimu kulingana na jinsia ili kuelewa athari tofauti za mgao wa bajeti na matokeo ya utekelezaji wa sera kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana pamoja na watu wenye mahitaji maalum. Hii inahusisha kuhakikisha kuwa mbinu za ukusanyaji taarifa ni jumuishi na zinaheshimu faragha na mahitaji ya makundi yote.

iii. Hakikisha ushiriki wa wadau katika makundi yote: Jumuisha makundi mbalimbali ya wadau kwa pamoja ili kupata maoni na uzoefu wao katika kutambua masuala muhimu ya kijinsia na kubuni hatua zinazofaa.

iv. Fanya uchambuzi wa kijinsia: Fanya uchambuzi wa kijinsia wakati wote wa mchakato wa tathmini na ufuatiliaji ili kutambua tofauti za kijinsia, na fursa za mabadiliko ya kijinsia. Uchambuzi huu unapaswa kutoa mwongozo wa kufanya maamuzi na kubuni programu ili kuhakikisha kuwa hatua zinazotolewa zinapelekea usawa wa kijinsia.

v. Fuatilia mgao wa bajeti na matumizi: Angalia mgao wa bajeti na matumizi ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinagawiwa kwa usawa na kutumika kwa ufanisi kutatua tofauti za kijinsia. Hii inahusisha kufuatilia mgao wa fedha kwa programu zinazojali makundi tofauti ya watu na kutathmini athari zake ili kupata huduma muhimu pamoja na fursa mbalimbali.

vi. Tumia mbinu za tathmini zinazojali jinsia: Tumia mbinu za tathmini zinazojali jinsia, kama vile mifumo ya uchambuzi wa kijinsia, viashiria vinavyozingatia jinsia, na mbinu za ushirikishwaji, ili kutathmini athari za bajeti kwa matokeo ya usawa wa kijinsia. Hii inahakikisha kuwa michakato ya tathmini inahusiana na mienendo ya kijinsia na inajumuisha uzoefu wa makundi mbalimbali.

Hamasisha ujifunzaji na kukuza uelewa: Jenga utamaduni wa kujifunza na kubadilishana uzoefu kwa kuandika taarifa na kujadili mambo yaliyojitokea kutokana na taarifa za tathmini na ufuatiliaji. Hii inahusisha kushiriki mbinu bora, hadithi za mafanikio, na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti yenye mrengo wa kijinsia ili kuongoza mipango na maendeleo ya sera ya baadae.

Kwa kutekeleza mikakati hii, Serikali, washirika wa maendeleo, na mashirika ya kiraia wanaweza kuimarisha usawa wa kijinsia na kuharakisha maendeleo yatakayo pelekea kuwepo kwa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake/wasichana na wanaume/wavulana.

### 3.4.7 HATUA YA 7: Kuandaa tamko la ukondoishaji wa masuala ya kijinsia katika uandaaji wa mipango na bajeti

Huu ni waraka mahsusi wa uwajibikaji wa kijinsia unaotolewa na Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuonyesha bajeti zake zinafanya nini kuhusiana na jinsia. Waraka wa bajeti ya jinsia huandaliwa baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuandaa bajeti na kutenga rasilimali kwa kulingana na mipango ya mwaka.

Kama ilivyo kwenye mipango na bajeti zenye mrengo wa kijinsia, waraka unazingatia mahitaji na vipaumbele vya makundi yote ya kijinsia katika jamii, jinsi yatavyoathiriwa na mipango na bajeti kwa mwaka husika. Waraka huu unaweza kwenda mbali zaidi na kuelezea maeneo ya kimkakati ya kijinsia ambayo yamezingatiwa katika bajeti iliyoandaliwa. Maeneo hayo ni kama;

i. Ushirikishwaji wa wadau mbalimbali

ii. Matumizi ya takwimu zilizonyumbulishwa kwa kuzingatia jinsi, umri na hali ya ulemavu

iii. Mgawanyo wa rasilimali uliozingatia usawa wa kijinsia

iv. Masuala ya kuwajengea uwezo wataalam mbalimbali katika eneo la bajeti yenye mrengo wa kijinsia

# 4. SURA YA NNE – MPANGO KAZI

Katika sura hii lengo mahsusi ni kuona namna washiriki wanavyotumia mafunzo waliyopewa katika kujaribu kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia. Mwezeshaji awaongoze washiriki kuandaa mpango kazi wa namna ambayo wataweza kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

**Zoezi la kumi na tatu**

Kuandaa Mipango Kazi

i. Washiriki wanapaswa kukaa katika vikundi na kuandaa mpango halisi wa utekelezaji wa mapungufu yaliyoainishwa wakati wa mafunzo.

ii. Washiriki wanapaswa kutumia masuala yaliyoainishwa katika Zoezi namba 3 katika somo la kwanza kuhusu mahitaji ya kijinsia ya vitendo na ya kimkakati ya wavulana na wasichana na watoto wenye mahitaji maalumu katika jamii yao.

iii. Washiriki wanapaswa kutumia njia ya uchambuzi wa mti wa tatizo ili kutofautisha sababu za msingi, tatizo la msingi na madhara ya masuala ili kusaidia katika kubuni afua zinazofaa, kuchagua viashiria muhimu ili kushughulikia mahitaji/ masuala ya kijinsia kwa wasichana na wavulana

iv. Tumia jedwali lililo hapa chini kujaza mpango kazi

v. Washiriki watawasilisha mipango yao ya utekelezaji kwa darasa ili kupokea maoni kutoka kwa washiriki wengine

## 4.1 Mpango kazi

| Vikwazo mbalimbali katika uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia | Shughuli ya kufanya kutatua kikwazo hiki? | Wahusika/ Wadau Muhimu? | Rasilimali muhimu | Muda wa utekelezaji | Matokeo/ viashiria vya mabadiliko |
|---|---|---|---|---|---|

## 4.2 Hitimisho

Bajeti yenye mrengo wa kijinsia si bajeti kwa wanawake pekee bali ni bajeti inayozingatia mahitaji ya jinsi zote. Takwimu na sauti za makundi yote ni muhimu kabla ya kupanga na kutenga fedha. Ufuatiliaji wa matokeo ya kijinsia ni hatua muhimu katika mzunguko mzima wa bajeti.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
Mtaa wa Afya, Mji wa Serikali, Mtumba.
P.O. Box 573, 40478 Dodoma, Tanzania.
www.jamii.go.tz

**Huduma kwa Wateja:**

**Namba za Simu:**
0734 986 503 / 0262 160 250

**WhatsApp:**
0766 400 168 / 0769 608 130

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
Mtaa wa Afya, Mji wa Serikali, Mtumba.
P.O. Box 573, 40478 Dodoma, Tanzania.
www.jamii.go.tz

**Huduma kwa Wateja:**
**Namba za Simu:**
0734 986 503 / 0262 160 250
**WhatsApp:**
0766 400 168 / 0769 608 130

Kwa Kushirikiana na:

In **partnership** with Canada

PLAN INTERNATIONAL
Until we are all equal